

TAARIFA KWA UMMA



BODI YA BIMA YA AMANA

KATIKA SHAURI LA FBME BANK (ILIYO CHINI YA UFILISI)

MALIPO YA FIDIA YA AMANA KWA WATEJA WA FBME (CHINI YA UFILISI)

Kufuatia uamuzi wa Benki Kuu ya Tanzania kuifutia **FBME BANK LTD** leseni ya kufanya shughuli za kibenki mnamo tarehe 8 Mei, 2017, Bodi ya Bima ya Amana inatangaza kuanza kulipa fidia ya bima ya amana kwa wenye amana katika **FBME BANK LTD** (Iliyo Chini ya Ufilisi) kuanzia tarehe 1, **Novemba, 2017**. Fidia hii inalipwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006.

1. Ili kufanikisha malipo ya fidia hiyo, wenye amana wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

(a) Mahali na Muda wa Malipo

Malipo ya fidia ya bima ya amana yatafanyika katika matawi yote ya iliyokuwa **FBME BANK LTD**, isipokua tawi la Samora ambalo wateja wake watalipwa kupitia tawi la Kinondoni. Muda wa saa za kazi utakuwa kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 10.30 jioni katika siku za Jumatatu hadi Ijumaa na kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 6.30 mchana kwa siku za Jumamosi.

(b) Ukomo wa Malipo ya Fidia

Kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, fidia ya bima ya amana ni hadi shilingi 1,500,000/-.

(c) Madai kwa amana zinazozidi Shilingi 1,500,000/-

Kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, kwa wale wenye amana zinazozidi Shilingi 1,500,000/-, watalipwa kwa mujibu wa utaratibu wa ufilisi kama itakavotangazwa.

(d) Viambatanisho vinavyohitajika

- (i) **Fomu ya Madai** iliyojazwa vizuri pamoja na nakala yake: Fomu hii inapatikana katika yaliyokuwa matawi ya **FBME BANK LTD** (Iliyo chini ya ufilisi) na katika tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania: www.bot.go.tz
- (ii) Kadi ya Utambulisho wa Mwenye Akaunti
- (iii) Utambulisho halisi wa mwenye amana kwa kuonyesha kimoja wapo kati ya; Kitambulisho cha Uraia, Hati ya Kusafiria, na kwa walio Watanzania, wanaweza kuwasilisha Leseni ya Udereva, Barua ya Utambulisho kutoka kwa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa/Sheha au kitambulisho cha mpiga kura.

2. Uchukuaji wa mali za wateja zilizopo katika kabati maalum (Safe Deposit Lockers);

Wateja wenye mali zao katika kabati maalum katika FBME Bank Limited (chini ya ufilisi) wanaweza kuja kuchukua mali zao na kurudisha funguo za kabati hizo kuanzia tarehe 1 Novemba 2017.

(d) Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:

**Mkurugenzi,
Bodi ya Bima ya Amana
Mtaa 2 Mirambo
S. L. P 2939
11884 Dar es Salaam
Simu: + 255 22 223 5390
Barua pepe: DIB-INFO@bot.go.tz**

Imetolewa na:

Mkurugenzi, Bodi ya Bima ya Amana
Tarehe 28 Octoba, 2017